# Maendeleo kwa Wote

Halmashauri ya Mji wa Njombe | Toleo Namba oo1,Septemba 2018


## Toleo Maalum la Utekelezaji Shughuli za TASAF



Uboreshaji wa miundombinu ya barabara >> uk 11



Namna ufugaji kuku ulivyowanufaisha walengwa wa TASAF >> 10



Zahanati za TASAF kuboresha Sekta ya Afya >> 07



## NDANI

Sekta ya afya yaimarishwa

TASAF III yapunguza Umaskini

Miundombinu ya Elimu yaboreshwa

Wajasiriamali wanufaika kupitia TASAF III

## Kutoka kwa Mkurugenzi



Illuminatha Mwenda
Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Njombe

Salaam Ndugu Msomaji,
Karibu katika Toleo la kwanza la Jarida la Maendeleo Kwa Wote ambalo hutolewa na Halmashauri ya Mji Njombe.
Toleo hili ni la kwanza katika Halmashauri ya Mji Njombe tangu ilipoanza utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Halmashauri ujulikanao kama TASAF III, 10 Novemba 2014.
Toleo hili linajumuisha shughuli za utekelezaji wa kazi mbalimbali za TASAF zilizofanyika katika Halmashauri ya Mji Njombe na pia linajumuisha habari za mafanikio zilizofikiwa na wanufaika wa TASAF katika Halmashauri na ni kwa jinsi gani wameweza kunufaika na mpango huu kwenye maeneo ya utekelezaji.
Kupitia Jarida hili utapata fursa za kuweza kufahamu ni kwa jinsi gani TASAF kwa kushirikiana na jamii husika inashiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya afya, elimu, na uboreshaji wa miundombinu ya barabara ili Taifa la Tanzania liweze kuwa na maendeleo endelevu na wananchi wake waweze kuwa na vipato maradufu kwa kushiriki katika mpango wa ajira za muda na uundwaji wa vikundi vya kuweka na kukopa.
Ni matumaini yetu msomaji wa jarida hili utafurahia makala zetu na kupata ufahamu wa yale yaliyojiri na kukonga nyoyo za wengi katika utekelezaji wa mpango wa Kunusuru kaya Maskini katika Halmashauri ya Mji Njombe.
Kwa taarifa zaidi usisite kutembelea Tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.njombetc.go.tz na kwa maoni yoyote na ushauri tutumie kwa barua pepe: td@njombetc.go.tz
Asanteni Sana.

## YALIYOMO

Utekelezaji wa Mpango wa kunusuru Kaya Masikini Halmashauri ya Mji......03
TASAF yasaidia ujenzi wa Zahanati Ramadhani uk......04
Kiwango cha fedha tunachopokea sio kidogo uk............06
TASAF kunufaisha Shule ya Msingi Madobole Njombe uk..........08
Wananchi waomba kupelekewa Miradi zaidi ya TASAF uk........11

## BODI YA UHARIRI

ILLUMINATHA MWENDA-MKURUGENZI

HYASINTA KISSIMA- MHARIRI MKUU

REVOCATUS RUGEIYAMU- MJUMBE

ZUFI NKANAWA- MJUMBE

ZUHURA ABDULRABI- MJUMBE

KENANI MALIGA-MJUMBE

LUKELO MSHAURA- MSHAURI

## ANUANI

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Njombe.
S.L.P 577 Njombe, Tanzania.
Simu ya Mezani: 026-2968833
Simu ya Mkononi: 0262968833
Barua Pepe: td@njombetc.go.tz
Tovuti: www.njombetc.go.tz

Gazeti hili pia linapatikana kupitia tovuti ya Halmashauri ya Mji wa Njombe ambayo ni www.njombetc.go.tz

# Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini TASAF III Katika Halmashauri ya Mji Njombe



*Wakusanya taarifa wakijaza dodoso la utambuzi wa kaya maskini kwenye mojawapo ya kaya iliyopitishwa\ kwenye mkutano mkuu katika kijiji cha Mgala Kata ya Ihanga Halmashauri ya Mji Njombe.*

Mpango wa kunusuru Kaya Maskini TASAF III ambao Kitaifa ulizinduliwa na Rais Mstaafu Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete Agosti 2012 mjini Dodoma, ulianza kutekelezwa katika Halmashauri ya Mji Njombe Novemba 2015 ukilenga kuzinusuru kaya maskini sana na zilizo katika mazingira hatarishi kupata mahitaji ya msingi ikiwemo Chakula, Afya na Elimu bila kusahau shughuli za uwekezaji ili kujipatia kipato endelevu.

Ifahamike kuwa, Mpango wa kunusuru kaya maskini umelenga katika maeneo makuu manne ambayo ni kuzinusuru kaya maskini. Hii inaenda sambamba na utoaji wa ruzuku kwa walengwa na mpango wa ajira za muda ambapo wanufaika hushiriki katika kazi za mikono na kujipatia kipato,pili uendelezaji wa miundombinu katika sekta ya afya,elimu,maji na barabara,tatu ni kuwawezesha wanufaika kuweka akiba na kuwekeza kupitia vikundi vidogo vidogo ambapo lengo lake ni kuwawezesha wanufaika kufuzu na hatimaye kutoka kwenye mpango na eneo la nne ni kujenga uwezo kwa wadau mbalimbali wa mpango.

Mpango huu ulianza kutekelezwa kwa kufanya utambuzi wa walengwa kupitia kwenye mikutano ya hadhara ambapo kwa kiasi kikubwa wanajamii katika kijiji husika waliweza kushiriki vyema kwenye kuwabaini wahusika kulingana na vigezo vilivyoainishwa.

Katika awamu ya kwanza ya utambuzi Halmashauri iliweza kufanya utambuzi wa walengwa 5462 ambapo mara baada ya zoezi la uchambuzi kufanyika kupitia mfumo maalumu, walengwa 3685 walikidhi vigezo na kuandikishwa kutoka katika vijiji 30 na mitaa 14 na kuingizwa kwenye mpango.

Mpango huu umekuwa na manufaa makubwa kwa wanufaika kwani wengi wameweza kuboresha maisha yao kadri siku zinavyokwenda kupitia ruzuku wanazopokea kila baada ya miezi miwili lakini pia kupitia ajira za muda wanazofanya za kuwaongezea kipato.

Kupitia mpango huu wa uhawilishaji fedha kaya nyingi zimeweza kumudu mahitaji muhimu kama chakula, mavazi, malazi lakini wanafunzi wengi ambao waliacha shule kutokana na familia zao kutojiweza kimaisha wamerudi shuleni na kuendelea na masomo.

Aidha, wanufaika wameweza kuanzisha miradi ya ufugaji na kilimo ambayo imekuwa ikiwaongezea kipato kwa namna moja au nyingine sambamba na kuboresha afya kwa kuhakikisha watoto chini ya miaka mitano wanahudhuria kliniki na kujiunga na huduma ya CHF ambayo imerahisisha upatikanaji wa matibabu kwa wanufaika wa mpango.

>>> UK 07

# TASAF yasaidia ujenzi wa Zahanati mtaa wa Ramadhani

Katika kuboresha huduma za afya Halmashauri ya Mji Njombe imeanza ujenzi wa zahanati katika Kata ya Ramadhani Halmashauri ya Mji Njombe. Zahanati hiyo ambayo hadi kukamilika kwake itagharimu zaidi ya milioni sitini na sita inajengwa kupitia mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) nchini ya ufadhili wa Muungano wa Mataifa yanayozalisha mafuta (OPEC) pamoja na nguvu za wananchi.

Afisa ufuatiliaji wa TASAF anayesimamia shughuli za mpango wa kunusuru Kaya maskini Halmashauri ya Mji Njombe, Revocatus Rugeiyamu alisema kuwa ujenzi wa zahanati hii pia itawezesha walengwa wa TASAF kutimiza masharti ya mpango.

"Miongoni mwa masharti ya mpango wa Kunusuru Kaya maskini ni kuhakikisha watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanapelekwa kliniki. Kwa kuliona hili TASAF kwa kufadhiliwa na OPEC ikaona ni jambo jema kujenga zahanati maeneo ambayo huduma hii haipatikani kirahisi. Alisema Rugeiyamu "Nina imani kuwa zahanati hizi zitatumika ipasavyo na walengwa watakua hawana sababu ya kujitetea kwa kutowapeleka watoto wao kliniki kwa kuwa zahanati zitakuwepo."Aliongezea Rugeiyamu. "Hii ndio TASAF tunayoiongelea haikuachi njiapanda inakuwezesha mlengwa kutimiza masharti ushindwe mwenyewe. Jambo la kufurahisha zaidi zahanati hii si manufaa ya walengwa wa mpango pekee bali hata wananchi wa eneo husika nao watanufaika zaidi."Alisema



*Jengo la Zahanati ya Ramadhan inayojengwa kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini TASAF III ambalo lipo katika hatua za umaliziaji*

Wakizungumza kwa nyakati tofauti tofauti wananchi wa mtaa huo ambao wamekuwa wakipambana kufa na kupona kuhakikisha wanafanikisha ujenzi wa zahanati hiyo walisema kuwa zahanati hiyo itasaidia kupunguza vifo vya kina mama na watoto kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wakati.

Joseph Mlowe ni mkazi wa mtaa wa Ramadhani ambaye pia ni fundi wa kujitolea kwenye zahanati hiyo alisema kuwa wananchi wa mtaa huo wamehamasika kushiriki kwenye ujenzi wa zahanati hiyo ili kukamilisha mradi kwa wakati na kuhakikisha mradi huo hauondoki katika mtaa wao.

"Tumeamua kujitolea kwa nguvu zetu zote ili kuhakikisha zahanati hii inakamilika kwa wakati. Tumekuwa tukichangishwa mara kwa mara fedha kwa ajili ya kugharamia pango la zahanati la sasa hali ambayo imekua ikileta usumbufu kwenye ukusanyaji wa michango."Alisema Mlowe

Mlowe aliongezea "Kukamilika kwa zahanati hii kutasaidi upatikanaji wa huduma kwa karibu hasa akina mama na watoto na kuinua uchumi na kipato cha wanajamii kwa kupunguza muda wa kufuata huduma za afya na kupata muda mrefu wa kuzalisha huku afya zikiimaraika."

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa wa Ramadhani, Bathromeo Kyando, aliiomba Halmashauri ya Mji Njombe kuhakikisha inawapatia wahudumu wa afya wa kutosha ili kuweza kutoa huduma bora zaidi kwani zahanati hiyo ni miongoni mwa zahanati zitakazokuwepo katika Kata za mjini na idadi ya watu ni kubwa ukilinganisha na maeneo ya vijijini.

Mradi wa ujenzi wa zahanati katika mtaa wa Ramadhan umegharimu kiasi cha shilingi milioni 66.706,980.51/= fedha ambazo zimetolewa na TASAF huku upande wa wananchi wakichangia mawe na tofali pamoja na kusaidia shughuli za ujenzi ikiwemo kubeba mchanga na kusaidia mafundi shughuli mbalimbali.

Kukamilika kwa zahanati hiyo kunataraji kuwahudumia zaidi wa wakazi elfu kumi na sita wa mtaa huo ikiwa ni sambamba na kuwawezesha walengwa kutimiza masharti na kusaidia jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya afya nchini.

# TASAF yajenga Nyumba ya Mwalimu Shule ya Msingi Umoja

Zipo changamoto mbalimbali zinazo ikabili Sekta ya Elimu Nchini licha ya Serikali kutumia rasilimali zake kuhakikisha sekta hiyo inazidi kuimarika siku hadi siku.

Mfano kwa siku za karibuni tumeona idadi ya walimu kutoka Shule za Sekondari wakihamishiwa katika shule za msingi ili kuleta uwiano sawa wa idadi ya walimu. Sambamba na hilo Serikali ya awamu ya tano kutoa elimu bila malipo ili kuhakikisha kuwa kila mtoto ambaye amefikia umri wa kwenda shuleni anapata elimu ikiwa ni sambamba na kuhakikisha kuwa shule zote zinapata madawati ya kutosha na kuondokana na tatizo la upungufu wa madawati.

Shule ya Msingi Umoja ni miongoni mwa Shule 76 za Msingi zinazomilikiwa na Serikali zilizopo katika Halmashauri ya Mji Njombe, ambayo tangu mwaka 2014 shule hiyo ilipoanzishwa imekuwa na nyumba moja tu ya Mwalimu ambayo inatumiwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo jambo linalowafanya walimu wengine 07 kupanga nje ya eneo la Shule.

Changamoto ya ukosefu wa nyumba za walimu katika shule hiyo pia iliwagusa Wananchi wa Kijiji cha Lugenge ambacho ndipo shule hiyo ilipo na kupendekeza mradi wa ujenzi wa Nyumba za walimu katika shule hiyo jambo ambalo TASAF hawakuwa na hiyana nalo.

Mara baada ya Kijiji cha Lugenge kuibua mradi huo TASAF ilianza mchakato wa ujenzi wa nyumba hiyo ambayo hadi sasa imekamilika kwa asilimia mia moja (100%) na inauwezo wa kubeba familia mbili za walimu "two in one"

Mwalimu Yeremia Mwilongo, ni Mwalimu Mkuu Msaidizi katika shule hiyo ambaye ameelezea manufaa ya nyumba hiyo na kufafanua kuwa itasaidia walimu kukaa maeneo ya jirani na shule. Alisema kuwa nyumba hiyo itawezesha walimu kuwasaidia wanafunzi katika muda wa ziada wa asubuhi au jioni tofauti na awali ambapo Mwalimu kukaa mbali na eneo la shule kunaleta ugumu wa kuwasaidia wanafunzi katika muda wa ziada.

Sambamba na hilo Mwalimu Yeremia alibainisha kuwa kutokana na kada ya walimu kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nyumba. Nyumba hiyo itaongeza morali ya kufanya kazi kutokana na uwepo wa makazi yaliyobora, huru na salama kwao.

Aidha, ameishukuru TASAF na kuiomba kufanikisha ujenzi wa nyumba za walimu zilizosalia na kuomba ujenzi wa darasa la awali kutokana na shule hiyo kutokuwa na darasa hilo.

Hadi kukamilika kwa ujenzi wa nyumba hiyo jumla ya shilingi milioni 63,017,818.75/= zimetumika na nyumba hiyo ina uwezo wa kubeba familia mbili na kupunguza tatizo la makazi ya Walimu katika shule hiyo.



*Muonekano wa nyumba ya mwalimu katika shule ya msingi Umoja iliyopo katika Kijiji cha Lugenge Kata ya Lugenge Halmashauri ya Mji Njombe iliyojengwa kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III.*

# "Kiwango cha Fedha tunachopokea sio Kidogo" Wanufaika wa TASAF Njombe.

"Nilianza na mbuzi mmoja, TASAF wakanipatia mbuzi wawili na nikafanikiwa kununua wengine wawili kupitia fedha za TASAF. Kwa sasa nina mbuzi watano nitaendelea na ufugaji wa mbuzi kwani tayari nimeona huu ni ufugaji mzuri na kwangu naona unatija". Hayo yalibainishwa na Galous Msagala mmoja wa wanufaika wa TASAF kutoka katika Kijiji cha Limage Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji wa Njombe ambaye hupokea kiasi cha Tsh. 32,000/= kwenye zoezi la uhawilishaji fedha kila baada ya miezi miwili.

Alisema Msagala kuwa wapo walengwa ambao wamekuwa wakipokea fedha na kuzitumia vibaya na kuwataka kuacha tabia hiyo badala yake wawekeze katika shughuli zinazowaletea maendeleo.

" Kwa kupitia fedha nazopokea toka TASAF lengo langu nikuwa na mbuzi wengi siko tayari kurudi nyuma tena" alibainisha Msagala.

Msagala amewataka wale wote wanaolalamika na kuona kiasi wanachopatiwa ni kidogo, kuwa na mipango mizuri ya fedha kwani kiasi hicho sio kidogo pindi unapokuwa unamipangilio mizuri na umeweka malengo.

"Fedha hii sio ndogo kinachotakiwa ni kuwa na matumizi mazuri na vipaumbele kama vile nilivyofanya mimi vinginevyo utakuwa mtu wa kulalamika na hautatoka kwenye umaskini" alisema Msagala.

Kwa upande wake Florence Mligo ambaye ni mjumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi katika Kijiji cha Limage alisema kuwa wanufaika wengi katika kijiji chake wamekuwa na mwamko mkubwa wa kufanya shughuli za maendeleo ikiwemo kilimo, ufugaji na wengine wameweza kuboresha makazi yao licha ya kuwa bado wapo wanufaika wengine ambao wamekuwa hawatilii mkazo yale wanayoambiwa.

"Kazi ya usimamizi ni ngumu lakini tunajitoa kwa moyo kuhakikisha wimbi la umaskini linaondoka kwa wanakijiji wenzetu na wao wanakuwa na maisha bora" alisema Mligo

Aidha, msimamizi huyo ameomba wataalamu wa mifugo na mazingira kutoa elimu maalumu ya maswala ya usafi wa mazingira kwa wanufaika kwani wengi wamekuwa wanafanya shughuli za ufugaji lakini wanashindwa kuandaa mazingira mazuri ya kufanya shughuli za ufugaji jambo



*Mmoja wa wanufaika wa TASAF kupitia mradi wa ufugaji mbuzi Bw. Galous Msagala akiwa pamoja na mifugo yake katika maeneo ya malisho Kijiji cha Limage Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji Njombe*

<<<uk 03

## Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

kwa sasa Halmashauri inajumla ya wanufaika 3422 mara baada ya kufanyika kwa zoezi la uhakiki sambamba na kuondoa wanufaika waliofariki au kuhama TASAF III imejikita katika shughuli za uibuaji wa miradi ambapo zoezi hili hufanyika kwa kuwahusisha wananchi wote kwa kufanya mkutano wa hadhara wa kijiji kwa kushirikiana na wanakamati. Katika Halmashauri ya Mji Njombe jumla ya miradi 21 imeibuliwa.

Miradi hii ni ile inayohusisha ukarabati wa mfumo wa maji,ujenzi wa nyumba za waalimu,madarasa,vyoo, ujenzi wa zahanati na miradi ya ufugaji ambapo jumla ya Tsh 1,094,021,091.61/= zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo

Zoezi la uhawilishaji fedha kwa wanufaika wa mpango lilianza Mwezi Septemba na Oktoba 2015 ambapo kufikia mwezi Agosti 2019 jumla ya Tsh.2,188,181,390 zimetolewa katika mizunguko 18.

Halmashauri ya Mji Njombe inajivunia na kuusifu mfuko wa maendeleo ya Jamii TASAF kwa kushirikiana katika utekelezaji wa mpango huu wa kunusuru kaya maskini na zilizo katika mazingira hatarishi kwani hii inaonesha wazi dhamira ya serikali ya kupiga vita umaskini nchini.

# Zahanati za TASAF kuboresha sekta ya afya Njombe

Wananchi wa Kijiji cha Ikisa Kata ya Uwemba Halmashauri ya Mji Njombe wamepongeza jitihada za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kufanikisha ujenzi wa Zahanati katika Kijiji hicho.

Wakizungumza na jarida hili wananchi hao walisema kuwa zahanati hiyo kwa kiasi kikubwa itapunguza vifo vitokanavyo na umbali wa kutafuta huduma za afya pamoja na gharama za upatikanaji huduma katika zahanati binafsi jambo ambalo limekuwa ni tatizo la muda mrefu katika kijiji hicho.

“Awali tulikuwa tukipata huduma za afya katika zahanati ya misheni ya Uwemba ambako wengi walishindwa kumudu gharama kubwa za matibabu. Umbali uliopo kutoka kijiji cha Ikisa mpaka kufika kituo cha Uwemba. Ili kufika Uwemba ni mwendo wa takribani nusu saa ukiwa na mgonjwa mwendo huu ni mkubwa sana na wengi hatuna uwezo wa kukodi magari. Zahanati hii ya Ikisa iliyojengwa na TASAF ni mkombozi mkubwa kwetu” Alisema Violet Sanga ambaye ni mkazi wa kijiji hicho.

Kwa upande wake Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji Njombe Daktari Thomas Ndalio amesema kuwa zahanati mbili zilizojengwa na TASAF III zitasaidia kutatua upungufu wa zahanati katika vijiji ambavyo havikuwa na zahanati kama Ikisa.

"Ningeomba kwa kipindi kijacho katika uibuaji wa miradi ya TASAF ni vyema ikafikiria maeneo yenye zahanati zisizo na vigezo.

"Katika kupanua wigo wa huduma za afya TASAF izifikirie zahanati zilizopo maeneo yaliyopo pembezoni na maeneo ya mpakani.Zahanati za Idihani,Itipula na Mamong'olo ambazo licha ya kuwa pembezoni hazikidhi vigezo vya zahanati na nyingine wamepanga katika majengo binafsi na ya serikali ya kijiji."Alisema Ndalio

Aliongezea kuwa yapo maeneo ambayo ni ya vipaumbele ambayo ni mtaa wa Mgodechi,Lunyanywi,Kihesa na Maheve ambayo nayo yanahitaji zahanati zilizo bora.

Akiongelea swala la vifaa tiba na wataalamu wa huduma za afya Ndalio alisema kuwa kwa mwaka 2018/2019 Halmashauri imepokea watumishi 53 ambao wataziba pengo kwenye maeneo yenye uhitaji na swala la vifaa tiba kwenye zahanati za TASAF tayari imejumuishwa kwenye bajeti. ya mwaka 2018/2019.

Zahanati ya Ikisa imegharimu jumla ya Milioni 64,768.161.52 na inataraji kuanza kutoa huduma siku za karibuni na kupunguza adha ya wananchi wa kijiji hicho kusaka huduma za afya





*Muonekano wa Zahanati ya Ikisa iliyopo katika Kijiji cha Ikisa Kata ya Uwemba Halmashauri ya Mji Njombe inayojengwa kupitia mradi wa kunusuru kaya maskini TASAF III.*

# Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF kuinufaisha shule ya Msingi Madobole Njombe

Wananchi wa Kijiji cha Madobole Kata ya Luponde Halmashauri ya Mji Njombe wameiomba Kamati ya usimamizi wa miradi ya jamii kuharakisha mradi mpya wa ujenzi wa nyumba za walimu na vyumba vitatu vya madarasa na matundu sita ya vyoo ili kurahisisha utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi katika shule hiyo.

Ombi hilo limetolewa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya msingi Madobole Jacob Mahundi iliyopo katika Kijiji cha Madobole Kata ya Luponde Halmashauri ya Mji wa Njombe alipokuwa akizungumza na jarida hili.

Mahundi alisema kuwa Shule hiyo ina upungufu wa nyumba saba za walimu, upungufu wa walimu watatu, upungufu wa matundu ya vyoo na uchakavu wa vyumba vya madarasa sita.

Alisema awali shule hiyo ilikuwa ikikabiliwa na upungufu wa madarasa mawili na ukosefu wa vyoo ambavyo vilikuwa vimetitia lakini waliishukuru TASAF kwa kuwajengea madarasa hayo na vyoo matundu sita mawili ya walimu na manne ya wanafunzi hali iliyonusuru shule hiyo kufungwa.

"Kweli tunaishukuru TASAF kwa msaada huu wa vyumba vya madarasa na vyoo kwa kuwa kabla ya mradi huu hali ilikuwa ni mbaya sana kwa kuwa ililazimika mikondo miwili kuwekwa kwenye darasa moja na kujikuta kila darasa likiwa na wanafunzi zaidi ya 70,"alisema Mahundi

Hata hivyo aliiomba serikali kuboresha vyumba vya madarasa vya shule hiyo kwa kuwa ni chakavu sana hali inayoondoa utulivu wa wanafunzi kujisomea vizuri.

Aliiomba serikali kuwa na mgawanyo sawa wa walimu kati ya mijini na vijijini na kuhakikisha angalau kila shule inakuwa na walimu wa kutosha ili kupunguza mzigo wa vipindi vya masomo kwa walimu.

Kwa upande wao wanafunzi wa shule hiyo wameiomba serikali kuwajengea jiko na bwalo la kulia chakula kwani wanafunzi hao hutumia vyumba vya madarasa kulia chakula ili hali vyumba hivyo vya madarasa huvuja na kuingiza maji kutokana na uchakavu wa shule hiyo.

Wakizungumza na jarida hili wanafunzi wa darasa la saba Studa Ndelwa na Derick Mlelwa waliiomba serikali kutatua changamoto ya maji, vifaa vya kufundishia, vitabu na waalimu kwa ujumla.

"Tunatatizo kubwa la vitabu hapa shuleni hali ambayo inawapa wakati mgumu walimu wetu namna ya kutufundisha lakini na sisi wanafunzi tunashindwa kujifunza vizuri hasa ikizingatiwa huku kwetu ni kijijini hatuna sehemu ya kwenda kuazima ama kujisomea kama ilivyo kwa wenzetu mjini," walisema.

Kukamilika kwa ujenzi wa madarasa mawili na matundu sita ya vyoo kunafungua njia ya kuanza kwa mradi mpya wa ujenzi wa nyumba mbili za walimu, ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu sita ya vyoo shuleni hapo kupitia TASAF III.Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini TASAF III umedhamiria kuhakikisha shule hiyo inakua na mandhari mazuri na inaondokana na changamoto ya uchakavu wa muda mrefu uliokuwa unaikabili shule hiyo.





*Picha ya kwanza kushoto ni jengo la zamani ikionesha hali halisi ya madarasa katika shule ya msingi Madobole kabla ya ujenzi wa mpango wa TASAF III.Picha ya pili kulia ni mwonekano wa sasa wa madarasa ya shule ya msingi Madobole mara baada kukamilika kwa ujenzi kupitia TASAF III.*

# Wanufaika wa TASAF Wajiunga na CHF



*Mwezeshaji Ngazi ya Halmashauri Bw. Hendry Kideula akitoa elimu kwa wanufaika wa TASAF kuhusiana na umuhimu wa kujiunga na CHF*

Hadi kufikia mwezi Agosti 2018 jumla ya wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini 2890 sawa na asilimia 84.5 kati ya wanufaika 3422 walikua wamejiunga na huduma ya bima ya afya ya jamii (CHF) katika Halmashauri ya Mji Njombe.

Akizungumza na jarida hili Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Mji Njombe, Zufi Nkanawa alisema kuwa wanufaika wengi wamejiungana huduma hiyo mara baada ya kupatiwa elimu ya umuhimu wa CHF.

“Halmashauri yetu imejitahidi kutoa elimu wakati wa malipo kuhusiana na umuhimu wa wanufaika kujiunga na huduma ya CHF na muitikio umekuwa ni mzuri" alisema Nkanawa.

"Tungeweza kufikia asilimia mia moja kwa kuwaunganisha wanufaika wote 3422 tatizo kubwa ni kwamba idadi iliyosalia tumeshindwa kuwaunganisha kwa sababu maeneo wanayotoka hakuna zahanati za serikali."alisema Nkanawa .

Aliongeza kuwa zahanati binafsi hawakubali bima hizi na kuiomba serikali kutatua changamoto hiyo ili walengwa wote wanufaike na huduma hii

Kwa upande wao wanufaika wa TASAF waliojiunga na huduma ya CHF walisema imekuwa na manufaa kwao wanapokuwa hawana fedha kwani wanaweza kwenda zahanati yoyote ya serikali na kutibiwa bure.

“Tunapoenda kwenye zahanati za serikali tunatibiwa bure, madawa yapo na huduma ni nzuri hamna ubaguzi wa aina yoyote tunafarijika sana”. Alisema Jane Mayemba ambaye ni mnufaika wa huduma ya CHF kupitia TASAF

Awali akizungumza na jarida hili Mayemba alisema kuwa mwamko wa wanufaika wa TASAF kujiunga na CHF umekuwa ni mkubwa sana ukilinganisha na hali ilivyokuwa awali kutokana na elimu ambayo wamekuwa wakipatiwa mara kwa mara ya umuhimu wa kujiunga na CHF.

Alisema kuwa awali tatizo lilikuwa ni ukosefu wa fedha za kujiunga na huduma hiyo, lakini kwa sasa kila mwezi wanauhakika wa kupata fedha hivyo hawaoni tabu kutoa kiasi kidogo kujiunga na CHF.

Wanufaika hao wamefurahishwa zaidi na uwezo wa CHF kuhusisha gharama kidogo za kujiunga na kuweza kuchukua idadi ya wanufaika 6 kwa malipo ya shilingi 10,000/=.

Aidha wameelezea kuwa moja ya changamoto zinazowakabili kwenye huduma ya CHF ni tatizo la kukosa huduma kwenye vituo binafsi kwa kutumia kadi zao za CHF na kuomba serikali kuwasaidia katika hilo.

Kwa upande wa Halmashauri ya Mji Njombe maeneo ambayo mpango wa kunusuru kaya maskini unatekelezwa na hayajafikiwa na huduma ya CHF kutokana na ukosefu wa zahanati za serikali ni Madobole,Uwemba,Uliwa,Ihanga, Mgendera na Lugenge.

# Namna ufugaji kuku unavyowainua wanufaika wa TASAF III



*Mradi wa ufugaji kuku wa mayai unaoendeshwa na Bi.Anna Ndawala ambaye ni mmoja wa wanufaika wa Mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III*

Anna Ndawala mkazi wa Kijiji cha Igominyi Kata ya Yakobi ni miongoni mwa mifano mizuri ya namna TASAF inavyowawezesha wananchi katika kuinua uchumi wao.

Bi anna ambaye anapokea kiasi cha shilingi elfu 32,000 kila baada ya miezi miwili aliingia kwenye mpango mwaka 2015.

Mara baada ya kuingia kwenye Mpango Anna alianza shughuli za ufugaji kuku mwanzoni mwa mwaka 2017 na alianza na ufugaji wa kuku 10 wa mayai. Kwa mwaka 2017 Anna alibahatika kuuza vifaranga katika awamu mbili tofauti na kujipatia kipato cha shilingi laki nane.

"Awamu ya kwanza niliuza vifaranga 120, awamu ya pili nikauza vifaranga 56 fedha nilizopata zilinisaidia kufanya shughuli mbalimbali. Nilifanikiwa kununua mahitaji ya shule ya mjukuu wangu, nilinunua mbolea ya kukuzia mahindi na zilinisaidia katika matumizi mbalimbali ya nyumbani. Nilifanikiwa pia kukarabati nyumba yangu na kuweka sakafu kwenye chumba ninacholala pamoja na kusakafia choo."Alisema Anna

Aidha, amefafanua kuwa licha ya kuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya mbinu za ufugaji bora na wakisasa kutoka kwa wataalamu wa mifugo na mbinu za kukabiliana na magonjwa lakini bado hajakata tamaa.

Sambamba na hilo Anna ameshauri ni vyema wasimamizi wa wanufaika wa mpango huu ambao ni wanakamati kuhakikisha wanawatembelea wanufaika mara kwa mara ili kukagua shughuli za maendeleo wanazofanya na kujiridhisha kwani wanufaika wengine wamekuwa si wakweli kwani pindi wapokeapo fedha za ruzuku wamekuwa wakizitumia hovyo badala ya kuwekeza katika shughuli za kuwaongezea kipato.

Kwa upande wake Mjukuu wa Mnufaika huyo ambaye anasoma darasa la tano katika shule ya Msingi Igominyi Agape amesema kuwa tangu walipoingia kwenye mpango amekuwa hakosi mahitaji muhimu ya shule kama viatu, madaftari, na ameendelea kufurahia maisha kwani hata katika familia wameweza kuboresha mlo kwa kula mayai na kitoweo cha kuku mara kwa mara jambo ambalo halikuwahi kutokea awali.

Kwa sasa Anna ambaye ni mnufaika wa TASAF III anakuku wa kienyeji wapatao 30 wa mayai 200 na kwa siku hukusanya mayai 150 ambayo ni sawasawa na Tray 5 za mayai.

Kufikia mwezi desemba mwaka 2018 Anna amedhamiria kukuza shughuli za ufugaji kuku, kutoka kuku 200 waliopo sasa mpaka kufikia kuku 700 jambo ambalo linamfanya kuishukuru TASAF III kwa manufaa aliyoyapata.

# Wananchi wa Igominyi Njombe waomba kupelekewa miradi zaidi ya TASAF

Wananchi wa Halmashauri ya Mji Njombe wamepongeza jitihada zinazofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Nchini (TASAF) kwa kuibua miradi na kuwapatia wananchi ajira za muda huku wakisukuma gurudumu la maendeleo na kuinua vipato vya mtu mmoja mmoja.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na jarida hili wananchi wa kijiji cha Igominyi Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji wa Njombe walisema kuwa miradi ya TASAF imekuwa na manufaa hususani katika maendeleo ya kijiji chao.

Daniel Ndonyalo ni mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Igominyi katika kijiji chetu kwa umoja na ushirikiano mkubwa hali ambayo imetufanya tubaki tukishangaa na kutamani kujiunga ili kuondoa kila changamoto iliyopo hapa kijijini,"alisema Ndonyalo.

Alisema kabla ya mradi huo wa barabara kuanza njia hizo zilikuwa ni korofi kiasi ambacho zilikwamisha maendeleo ya wanakijiji kwa kushindwa kusafirisha mazao ya biashara ili kuyafikisha sokoni.

Aidha aliiomba serikali kuunga mkono jitihada hizo za wananchi na kuhakikisha miradi hiyo ikiwezekana inaingia kwenye kila kijiji ili kujiharakishia maendeleo

Kwa upande wake mwenyekiti wa kijiji cha Igominyi Twilumba Salingwa alisema kupitia miradi ya TASAF wananchi wa kijiji chake wameweza kuimarisha vipato vyao lakini pia kujenga umoja na ushirikiano.

Alisema serikali ina mpango wa kuziunganisha barabara zilizoibuliwa na mradi wa barabara wa TASAF kuunganishwa kwenda kwenye kiwanda cha chai cha Lwangu ili kurahisisha usafirishaji wa zao hilo.

"Mimi nashauri mradi huu ukiisha uanzishwe mwingine ili kuendelea kuboresha vipato vya wananchi wangu ambao wengi



*Baadhi ya walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na TASAF katika Kijiji cha Igominyi Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji Njombe wakishiriki katika kazi za ujenzi w barabara kupitia mpango wa ajira za muda PWP*

ambaye alikiri kushuhudia miradi mbalimbali iliyoibuliwa na TASAF kupitia mradi wa kaya masikini na kukiri kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa umakini na ustadi wa hali ya juu.

"Nimeshuhudia wazee na wanawake wakifanya ukarabati wa barabara za kilomita 3.6 yao badala kusubiri viongozi na serikali pekee.

Mradi wa kaya masikini umekuwa na manufaa katika Kijiji cha Igominyi kwani wanufaika wengi wamejikwamua kwenye wimbi la umaskini uliokithiri sambamba na kuboresha miundombinu.

wameonekana kunufaika na miradi hii ambayo imewainua sana kiafya na kiuchumi pia,"Aliongeza Bi. Mgeni.

Wananchi hao wamekuwa wakishiriki katika miradi ya ajira za muda za TASAF kwa muda wa masaa manne kwa siku na hulipwa kiasi cha Shilingi 2300

# TASAF Yawanufaisha Wajasiriamali Wadogo Halmashauri ya Mji Njombe

Upo usemi wa kiswahili unaosema mgeni Njoo Mwenyeji apone ukiashiria kuwa mgeni anapotembelea, mwenyeji hupata kufaidika kwa njia moja au nyingine. Usemi huu umejidhihirisha wazi kwa wajasiriamali wadogo hususani katika maeneo ambayo vijiji vyao vimeingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini.

Wakizungumza kwa wakati tofauti tofauti na jarida hili, wajasiriamali hao ambao wengi wanafanya shughuli za kujiingizia kipato ikiwemo uuzaji wa vifaa vya ujenzi na mahitaji ya nyumbani wamesema kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa ukilinganisha na hali ilivyokuwa kabla ya vijiji vyao kuingizwa kwenye mpango.

Longinus Msemwa ni miongoni mwa wajasiriamali wadogo katika kijiji cha Madobole Kata ya Luponde ambaye yeye amefafanua kuwa kwa sasa biashara yake imeendelea kuimarika na uaminifu wa wateja wake hususani wanufaika wa TASAF umeongezeka kwani uhakika wa kuchukua mahitaji na kuja kulipa baadae ni wa uhakika kulingana na ruzuku wanazopokea. “Zamani kabla ya utambuzi na kijiji chetu kuingizwa kwenye mpango, ilikua ngumu kwa mimi kama mjasiriamali kumkopesha mnufaika wa TASAF mahitaji, hii ni kutokana na hali zao kuwa duni sana. Ukiangalia hali ya mtu ya kimaisha ilivyo unaona hata kama ukimkopesha atakulipaje? Hapo ndipo palipokuwa na kitendawili kwa maana unaona hana uwezo wa kukulipa.Kwa sasa baada ya kuingia kwenye mpango na kuanza kupokea ruzuku una uhakika wa kulipwa hata wakija walengwa hapa dukani kwangu nawakopesha."Alisema Msemwa Aliongezea kuwa "Wanapokea ruzuku, lakini pia wapo na ajira za muda ambazo zinawaingizia kipato hivyo sina wasiwasi na mimi biashara yangu inakua kupitia wao”.

“Wapo ambao kila wanapopokea ruzuku zile za kila mwezi huwa wananunua mahitaji yao hapa hao pia ni wateja wangu wazuri” Msemwa alihitimisha.

Furaha Mdendemi ni mfanyabiashara anayepatikana katika Mkoa wa Njombe Halmashauri ya Mji Njombe na biashara yake kubwa ni ya uuzaji wa vifaa vya ujenzi. Furaha ameweka bayana kuwa kupitia TASAF III ameweza kuingiza kipato cha uhakika kwani amekuwa akifanya biashara ya kuuza vifaa mbalimbali vya ujenzi.

“Nimenufaika sana kupitia mpango huu. Nimeuza vifaa mbalimbali vya ujenzi kama vile saruji, rangi,bati kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya TASAF. Kunapokuwa na miradi ya aina hii inakuwa ni neema kubwa kwetu kwani si rahisi kumpata mteja wa kawaida ambaye atachukua mahitaji mengi kwa wakati mmoja."Alisema Furaha.

Kwa upande wake Mratibu wa Mpango wa kunusuru kaya maskini Halmashauri ya Mji Njombe Zufi Nkanawa amesema kuwa kupitia TASAF III wanufaika wa mpango hupatiwa elimu ya ujasiriamali na jinsi ya kuanzisha miradi jambo ambalo limekuwa na manufaa makubwa kwao.

"Wanufaika wa Mpango katika Halmashauri ya Mji Njombe wamekuwa wakihamasishwa kuanzisha vikundi vya ujasiriamali kupitia fedha wanazopata kwa kujiwekea akiba na kukopeshana wao kwa wao"Alisema Zufi

Wajasiriamali hao wameishukuru TASAF kwakuwa manufaa ya mpango huo sio kwa walengwa pekee badala yake imeongeza mzunguko wa fedha katika vijiji husika na wao kuendelea kukuza mitaji ya biashara zao.



*Wauzaji wa vifaa vya ujenzi hunufaika kupitia miradi ya ujenzi inayotekelezwa kupitia TASAF III.Picha kutoka Maktaba*



*Wanufaika wa TASAF III katika Kijiji cha Igominyi Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji Njombe wakishiriki katika kazi za ujenzi wa barabara kupitia mpango wa ajira za muda PWP*



*Muonekano halisi wa vyumba vya madarasa katika shule ya msingi Madobole iliyopo Kijiji cha Madobole Kata ya Luponde Halmashauri ya Mji Njombe. Shule hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya Uchakavu wa miundombinu pamoja na ukosefu wa nyumba za walimu.*



*Mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III kupitia miradi ya OPEC imekamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Madobole, na sasa inataraji kuanza mradi mpya wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa, matundu sita ya vyoo sambamba na ujenzi wa nyumba mbili za walimu*

# HABARI KATIKA PICHA





*Wakusanya taarifa wakijaza dodoso la utambuzi wa kaya maskini kwenye mojawapo ya kaya iliyopitishwa\ kwenye mkutano mkuu katika kijiji cha Mgala Kata ya Ihanga Halmashauri ya Mji Njombe.*



*Mojawapo ya kaya maskini iliyopitishwa kwenye mkutano mkuu ikijaziwa dodoso la utambuzi wakati wa zoezi la utambuzi wa kaya maskini lililofanyika katika Kijiji cha Mgala Kata ya Ihanga Halmasahuri ya Mji Njombe*



*Mradi wa ufugaji kuku wa mayai unaoendeshwa na Bi.Anna Ndawala ambaye ni mmoja wa wanufaika wa Mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III*

# HABARI KATIKA PICHA





*Mwezeshaji ngazi ya Halmashauri ndg. Hendry Kideula akitoa elimu kwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III juu ya umuhimu wa kujiunga na bima ya afya CHF*

*Mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi ya mwalimu ukiendelea katika shule ya msingi Mwembetogwa iliyopo katika kijiji cha Mtila Halmashauri ya Mji Njombe.Ujenzi huo umefadhiliwa na OPEC kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III*





*Muonekano wa sasa wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi ya mwalimu katika shule ya msingi Mwembetogwa Halmashauri ya Mji Njombe, mara baada ya kukamilika kwa ujenzi uliofadhiliwa na OPEC chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III*

# HABARI KATIKA PICHA





*Mwonekano wa barabara ya Ihanga-Kilocha yenye urefu wa KM 6.8 iliyokarabatiwa na wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III katika Kijiji cha Ihanga, Kata ya Ihanga Halmashauri ya Mji Njombe.*

*Matundu ya vyoo yaliyokuwa yakitumiwa na wanafunzi wa shule ya msingi Madobole ambapo kutokana na uchakavu wa miundombinu katika shule hiyo yalipelekea kutitia kwa vyoo hivyo.*






*Matundu manne ya vyoo vya wanafunzi yaliyojengwa kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III katika shule ya msingi Madobole Halmashauri ya Mji Njombe.*